HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

Shule ya sekondari Nyaluhande,
S.L.P. 323,
Busega.

Kumb. Na. NYSS/S2102/J.14/11 15/12/2020

Mzazi/Mlezi wa …….
Shule ya msingi …….

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYALUHANDE WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI

Napenda kukupongeza kuchaguliwa kujiunga na shule hii kwa masomo ya kidato cha kwanza mwaka 2021. Ni matumaini yangu kuwa utaitumia nafasi hii vizuri kwa kujifunza kwa bidii ndani na nje ya darasa wakati wote uwapo shuleni.

Shule ya sekondari Nyaluhande imejengwa kwa juhudi za wananchi wa kata ya Nyaluhande. Hivyo ni vema kuitumia nafasi uliyopewa na kuthamini juhudi za wananchi, kujifunza kwa bidii kwa faida yako, familia, jamii na Taifa kwa ujumla.

Shule ya sekondari Nyaluhande ni ya kutwa pia ni ya mchanganyiko wasichana na wavulana. Imejengwa katika kijiji cha Nyaluhande.

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/01/2021

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE YA SHULE

- **WASICHANA**

i. Shati mbili nyeupe mikono mifupi za tetroni/tomato
ii. Sketi mbili za kitambaa kizito za rangi ya damu ya mzee zenye mchirizi mweupe katikati na iwe ndefu kufikia kifundo cha mguu. Sketi iwe na muudo wa linda boksi mbele na nyuma, jumla ya malinda yawe kumi. Aina ya kitambaa kimeambatanishwa.
iii. Tai yenye kufanana na rangi ya sketi
iv. Jozi mbili ya viatu vya ngozi nyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu
v. Jozi mbili za soksi nyeupe
vi. Bukta na fulana (T-shirt) rangi njano kwa ajili ya michezo
vii. Raba ya rangi yoyote kwa ajili ya michezo
viii. Sweta rangi ya bluu

- **WAVULANA**

i. Shati mbili nyeupe mikono mifupi za tetroni/tomato
ii. Suruali mbili za kitambaa kizito za rangi ya damu ya mzee, Suruali isibane mwili, iwe na linda moja kila upande. Aina ya kitambaa kimeambatanishwa.
iii. Tai yenye kufanana na rangi ya suruali.
iv. Jozi mbili ya viatu vya ngozi nyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu

v. Jozi mbili za soksi nyeupe
vi. Bukta na fulana (T-shirt) rangi njano kwa ajili ya michezo
vii. Raba ya rangi yoyote kwa ajili ya michezo
viii. Sweta rangi ya bluu

3.0 VIFAA VYA KUJIFUNZIA SHULENI

Unatakiwa kuwa na madaftari yasiyopungua tisa (09), kalamu za wino na mkaa, mkebe wa hesabu (mathematical set), rula na begi zuri la kubebea na kutunzia madaftari.

4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c) Kushiriki kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na zingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
i) Kutunza mali za umma.

4.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule
g) Kudharau bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
i) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

5.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANYAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA NMWANAFUNZI

i. Fomu ya kupima afya “Medical Examination Form” ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa shuleni kwa mkuu wa shule wakati utakaporipoti

ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII

……..

DANIEL S MALIMI

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI NYALUHANDE

NYALUHANDE SECONDARY SCHOOL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR A STUDENT SELECTED TO JOIN FORM ONE YEAR 2021

THE MEDICAL OFFICER

……..

……..

……..

Name of student ……

Please examine the above mentioned as to his/her fitness for Secondary Education according to the following items below:

No.	ITEM	CONDITION	REMARKS
1	Mentally		
2	Sight		
3	Hearing		
4	Chest		
5	Urine		
6	Stool		
7	Nose		
8	Blood (BP, HP)		
9	Pregnancy		
10	Others		

Any other disability not listed that may affect his/her studies

……

……

……

REMARKS

……

……

……

SIGNATURE ……. Official Rubber stamp

DESIGNATION ……..

DATE ……..

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

SHULE YA SEKONDARI NYALUHANDE
HISTORIA YA MWANAFUNZI

Jaza fomu hii na kuileta shuleni

1. Jina la ukoo …… Jina la kwanza …….. Jina la kati ……
2. Jina la mzazi/mlezi ……
3. Kama ni mlezi, taja uhusiano …… Namba za simu ……
4. Anwani ya kudumu ya mzazi/mlezi ……..
5. Mahali mwanafunzi anapoishi: Kitongoji ……. Kijiji ……
   Kata ya …… Wilaya ya …… Mkoa wa ……
6. Dini ……
7. Unaingia Kidato cha …….. tarehe ……..
8. Kutoka shule ya msingi ……..... Wilaya …….. Mkoa ……..
9. Kazi ya Mzazi/Mlezi wako: Mfanyakazi/ Mkulima/Mfanyabiashara …… mahali ……..
10. Usafiri unaotumia kutoka hapa shuleni hadi nyumbani kwenu ni (Taja) ……
11. Umbali kutoka hapa shuleni hadi nyumbani kwenu ni kilometa ……
12. Taja ndugu wengine ambao wanaweza kupelekewa habari muhimu juu yako /masuala ya shuleni
    i …….. Uhusiano …… Namba za simu ……
    ii …….. Uhusiano …… Namba za simu ……
    iii …….. Uhusiano …… Namba za simu ……
13. Kabla hujaja hapa shuleni umewahi kupimwa na Daktari? **NDIYO/HAPANA** Kama ni **ndiyo** ni ugonjwa upi wa kudumu ulio nao? ……
14. Taja sifa maalumu ulizonazo ……..
15. Taarifa za wazazi: wapo hai …… Wamefariki …… (Jibu ndiyo au Hapana)

Nathibitisha kwamba maelezo niliyoyatoa hapo juu ni sahihi.

…… ……

Saini ya mwanafunzi Saini ya mzazi/Mlezi

AHADI YANGU, Mimi (Jina la mwanafunzi) ……. nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na Shule hii, naahidi kufuata sheria za shule na taratibu zote kama zilivyotolewa na uongozi wa shule.

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi) ……. ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……. nimeyasoma maelekezo na sheria za shule ya sekondari Nyaluhande , ambako mtoto wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mtoto wangu kufuata sheria na taratibu zote za shule. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mtoto wangu ili baadaye awe raia bora na mwema kwa jamii na Taifa letu.

Saini ya mwanafunzi …….. Saini ya Mzazi/Mlezi ……

Jina la mwanafunzi …… Jina la Mzazi/Mlezi ……

Tarehe …….. Tarehe ……